# Ubatizo wa maji

**Utangulizi**

Ni muhimu kuisoma Biblia kujifunza Mungu anayoyasema kwa watu wake. Ninaamini katika kuyachunguza maandiko vizuri ili kujua hasa yale Mungu anayo kwetu.Mungu hasema neno lake ni roho na uzima .Linaleta uzima kwa wale wamtafutao kwa bidii na kulitii neno lake . Ni muhimu sana kuwa na ukweli wa Mungu katika nyanja zote za maisha yetu.

Nilikuwa katika kanisa lililoamin neno la mungu. Chochote Mungu alinena hakikubadilishwa. Nilikulia katika dhehebu kubwa nikafunzwa kupitia dhehebu hilo na kukua katika neno la Mungu . Nilienda katika shule ya parokia(msingi), shule ya upili, chuo na seminari

Wakati wote huo niliokuwa katika shule hizi na kwa sababu ya malezi yangu, nilijifunza kuwa lazima nimtii Mungu kulingana na neno lake na kumwamini . Ninamshukuru Mungu sana kwa sababu ya malezi yangu. Lakini jinsi nilivyoanza kulitafuta neno la mungu nilipata kukiwa na makosa kuhusiana na yale niliyofunzwa na vile Bibilia inavyosema.

Ninaamini ni muhimu sana kuchunguza maandiko vizuri ili kupata yale anayoyasema Mungu kuhusu mambo mbalimbali.Wakati nilipokuwa mchungaji wa kanisa la kawaida,Mungu alinena ndani ya moyo wangu. Niliweza kuhisi kuwa Mungu alikuwa akinena kuhusu ubatizo.

Kabla ya tukio hili nilikua nikihisi kuwa nilihitaji kubatizwa kwa maji.Sikuweza kuelewa hisia hii ndani yangu, kwa hivyo nikauliza Mungu kuihusu nikisema, “Bwana, mimi nimebatizwa tayari” kutokana na malezi tuliyopewa sisi tulibatizwa kama watoto wachanga, Kwa hivyo niliuliza Mungu kwa undani kuhusu haya naye akanihudumia kuhusu ubatizo wa maji. Yote yanayohusiana nao na ni akina nani wanapaswa kubatizwa.

Ninataka kushiriki mambo haya nanyi. Angalia katika Biblia yako na uchunguze maandiko haya ili kuhakikisha yale tunayoshiriki ni yale ambayo Mungu anayosema. Ni muhimu kutochukulia jambo kuwa la kweli eti kwa sababu mtu amekwambia ni ukweli. Lichunguze mwenyewe katika mwelekeo wa neno la Mungu.

Neno la Mungu linadhihirisha wazi kuwa watu wanapaswa kubatizwa kwa maji. “*Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la baba, na la mwana, na la roho mtakatifu*”(Mathayo 28:19) katika Matendo ya Mitume 2:38 watu waliuliza, “*Tutendeje, ndugu zetu?*” naye petro akawaambia,”*tubuni mkabatizwe....... mpate ondoleo la dhambi zenu*.”

Ule mwito mkuu ni wa kuenda na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi na kuwabatiza . unasema”*Watakaoamini na kubatizwa wataokolewa,wasioamini watahukumiwa.*”(Mariko 16:15,16)

## NJIA IFAAYO YA UBATIZO UFAAO

Neno la Mungu halisemi ni wakati gani au umri gani mtu anapaswa kubatizwa, kwa kuwa kuna mapenzi ya mtu na imani ya kuupokea ubatizo kama sehemu mtu ya kuutimiza. Hata hivyo kuna njia zifaazo za ubatizo ufaao ambazo zimedhihirishwa. Mtu anapaswa kufanya nini kabla ya kubatizwa?.

1. Kitu cha kwanza mtu anchokihitaji ni kufunzwa neno la Bwana (Tazama tena Mathayo 28:19,Mariko 16:15-16) Katika nyumba ya Kornelio watu walifunzwa na kulipokea neno la Mungu na pia wakajazwa Roho Mtakatifu. (Matendo ya Mitume 10:43-48) Roho Mtakatifu aliwashukia na wakasema kwa lugha na kutabiri.Swali liliulizwa,"*Ni nani awezaye kuzuia maji,hawa wabatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi*" Tunajifunza kuwa kabla ya ubatizo lazima watu wafundishwe. "*Basi,enendeni,mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"*. Mafunzo huja kabla ya ubatizo.Neno linaendelea kusema, "*Mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.*"
2. Jambo la pili ni kutubu kabla ya kubatizwa.Matendo ya Mitume 2:38 yasema kuwa mtu anahitaji kutubu kabla ya kubatizwa. Kutubu kunamaanisha kutoishi kwa ajili yako mwenyewe na shetani na kumrudia na kumtii Mungu, Mungu akiwa tumaini lako.
3. Jambo la tatu kuhusu ubatizo wa maji ni kumpokea na kumkiri Yesu Kristo kama Bwana(kwa kinywa chako).Tazama matendo ya Mitume 16:31-33,Warumi 10:9-10, Matendo ya Mitume 8:29-39 na Matendo ya Mitume 8:12)

Roho wa Mungu alikuwa akinihudumia kuhusu ubatizo wa maji nami nilikuwa nikimwambia,"Bwana mimi nilibatizwa nikiwa mtoto mchanga. Sasa kwa nini nahitaji kubatizwa tena?"Nilifikiria kuwa nitakuwa nikibatizwa tena. Hakika Biblia inasema kuhusu ubatizo mmoja wa maji. (Waefeso 4:5) kwa hivyo ni kitu gani tunakabiliana nacho? Kanisa limefunza kwa karne nyingi kuwa mtoto anatakiwa kubatizwa. Kwa hivyo ufanye nini?. Je, ni ubatizo mwafaka?.

Roho wa Mungu alipoanza kunihudumia,Bwana aliniuliza maswali kadha. Aliuliza,"Ni jambo gani linaloufanya ubatizo kuwa mwafaka? Nami nikampa neno la Mungu kuhusu kutubu na kubatizwa.

Alisema, "Je, ulitubu ulipokuwa mtoto?(Kutubu ni kuziona dhambi zako,kuziacha na kumgeukia Bwana.

Nikasema,"La sikutenda hayo"

Aliendelea,"Imani huja namna gani?"(Imani inahitajika ili kupata ubatizo mwafaka. Mtu lazima amwamini Bwana Yesu Kristo.)

Nikamwambia,"Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.(Warumi 10:17)

Aliniuliza,"Uliwahi kulisikia neno la Mungu ukiwa mtoto?"

Nikamjibu, "La, sikuwahi kusikia neno la Mungu. Nilibatizwa nikiwa na umri wa wiki tano au sita".

Aliniuliza,"Ikiwa hukulisikia neno la Mungu, ulikuwa na imani?"

Ilinibidi niseme,"La, sikuwa na imani yoyote"

Aliendelea,"Ikiwa imani ni kigezo cha kuufanya ubatizo uwe mwafaka,basi hukuwa na imani yoyote ?

Nikasema,"Wazazi wangu walikuwa na imani."

Alielezea,”Wazazi wako kuwa na imani ni jambo sawa na zuri lakini wewe hukuwa na imani”

Jambo moja tunalojifunza kutoka neno la Mungu ni kuwa bila imani hatumpendezi Mungu kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko,kwamba huwapa thawabu wale wamfuatao(Weabrania 11:6)

Desturi katika Kanisa la kwanza ilikuwa kuwaweka wakfu watoto mbele za Bwana. Wazazi walifanya hivi na jambo hili lilikuwa zuri kwa sababu watu wa Mungu ni lazima wawalete watoto wao mbele za Mungu. Wampatie Mungu,wawatie wakfu na watafute baraka za Mungu juu ya watoto wao. Hivyo ndivyo wazazi wangu walifanya kwa kumtii na kumpenda Mungu na kunipenda. Hata hivyo jambo ni hili,huo ulikuwa ubatizo ufaao kulingana na neno la Mungu?.

Kama Mungu alivyoendelea kunihudumia,aliniuliza,”Ulitakiwa kufanya nini ili kupokea wokovu? Nilimjibu,”Niliamini katika moyo wangu kuwa Yesu Kristo`ndiye Bwana na nikakiri kwa kinywa changu,”Yesu Kristo ndiye Bwana”na nikaamini katika moyo wangu kuwa alifufuka kutoka wafu.(Warumi 10:9-10)

Aliniuliza,”Umekiri kwa kinywa chako kuwa Yesu Kristo ni Bwana wakati ulipokuwa mtoto ukibatizwa?

Nikamjibu,”La, kwa maana singeweza hata kuongea.” Mungu alikuwa akitaka kunionyesha kuwa vigezo vyote vya kibiblia vya ubatizo ufaao kulingana na neno la Mungu (kama , imani katika Yesu,kumkiri Mungu na kutubu), havikufuatwa nami kama mtoto mchanga. Lakini kanisa limefundisha kuwa niliupokea ubatizo kwa njia ifaayo.

Tena, Matendo ya Mitume 2:38 yasema,”*Tubuni mkabatizwe*” singetubu kama mtoto. Neno la Mungu linasema katika warumi 10:9-10, “*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako, ya kuwa ni Bwana ,na kumuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu,utaokoka*” Nikiwa mtoto wa wiki tano au sita singeweza kuongea. Watoto wengi hawawezi kuongea mpaka watimize umri wa mwaka mmoja.

Tunatakiwa kuyapima yaliyotendeka katika maisha yetu kwa msingi wa neno la Mungu. Nakutia changamoto uweze kuyachunguza maandiko yanayohusiana na ubatizo pamoja nami. Najua katika tajriba yangu na katika moyo wangu kuwa ubatizo nilioupokea kama mtoto haukuwa ubatizo ambao Mungu anazungumzia katika Bibilia.

Wakati neno la Mungu lilinijia katika nyanja hizi na nikaanza kuzitazama kwa uangalifu sana, nilienda na kubatizwa kwa maji nikimwamini Bwana Yesu jinsi Biblia inavyoagiza kama alivyofanya Yesu kwa utakatifu wote.

## KUTIWA WAKFU KWA WATOTO

Yesu aliwekwa wakfu akiwa mtoto mchanga wakati alipelekwa hekaluni na wazazi wake. Lakini katika umri wa miaka thelathini alibatizwa na Yohana mbatizaji. Yesu aliyasema haya wakati huo, “*Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kutimiza haki yote”*. (Mathayo 3:15). Ni jambo la kumtii na kumpenda Mungu.

Tena nikamuuliza Bwana, “Nao watoto ni jinsi gani? Kunafanyikaje kwa wale watoto wachanga? Alinipatia neno katika 1 Wakorintho 7:14, lisemalo imani ya wazazi wanaoamini huwakinga watoto mpaka wafike umri wa kuweza kumpokea Bwana Yesu Kristo.

Hii ni zawadi kubwa sana umezawadiwa na Mungu,Nafasi ya kuwa mzazi anayeamini, ukimpenda mtoto wako na kumkabidhi Mungu mtoto wako. Ninaamini katika kuwaweka wakfu watoto hao. Ninaamini kuwa baraka spesheli za Mungu zaweza kuwa juu ya watoto kupitia wazazi wanaoamini. Lakini kuna wakati ufikapo na hakuna atakayeweza kusimama mbele za Mungu na kusema, “Ninabebwa kwa imani ya wazazi wangu” ama “Ninabebwa kwa imani ya mtu mwingine”

Kila mtu anatakiwa kujitolea Mungu yeye mwenyewe. Imani inatakiwa iwe katika moyo wa kila mtu. Siwezi kumlaumu mwingine, Siwezi kumsifu mwingine. Lazima nisimame mbele ya Mungu na kusema, “Yesu Kristo, wewe ni Bwana wangu . Kama ulivyofufuka kutoka kwa wafu, nami nimefufuliwa kutoka wafu na kuingia uzimani.

## UBATIZO WA MAJI HUWAKILISHA NINI

Ubatizo wa maji ni ishara inayoonyesha kazi nzuri inayotendwa na Roho wa Mungu ndani ya watu wake  na kuwafanya wapokee uzima. Uzima wa Mungu unawajia wanapoingia majini, mtu wa kale ambaye hampendi au kumjali Mungu hufa na kuzikwa na Yesu. Wanapotoka kwenye maji hayo, kama Yesu alivyofufuka  kutoka wafu, wanafufuliwa katika uzima.

Tunaona katika neno la Mungu katika kila kisa kinachorejelewa, kabla ya watu kubatizwa kwa maji, kwanza walisikia neno na wakalipokea kwa kutubu na kumuamini Bwana Yesu Kristo. Walikiri kwa vinywa vyao kuwa Yesu ndiye Bwana wao.

Imani ndiyo inayookoa mtu. Mtu aaminiye na kubatizwa ataokoka. Anayeamini ataokoka, lakini yule asiyeamini atapotea. (Mariko 16:14), Iimani humjia mtu kwa kusikiliza neno la Bwana kama tulivyoona katika Warumi 10:17. Ikiwa imani haimo kwa anayebatizwa basi hakuna ubatizo lakini ni kuoshwa tu kwa maji bila faida yoyote ya kiroho.

Ukitaka kumtia wakfu mtoto wako mbele za Bwana ukitumia maji kama ishara,basi hivyo ni vyema . Lakini huu si ubatizo ambao Biblia huzungumzia. Desturi ya wazazi au waakilishi wao kuamini kwa niaba ya mtoto mchanga katika ubatizo wake si desturi ya kimaandiko na hakuna neno linaloshikilia desturi hii. Kwa maneno mengine hakuna anayeweza kumwamini Mungu kwa niaba yako. Lazima umuamini Mungu wewe mwenyewe.

## MUNGU AMERUHUSU KUBATIZWA KWA WATOTO WACHANGA

Inafikiriwa mara nyingi kuwa Yesu aliruhusu watoto wachanga kubatizwa wakati alisema,”*Wacheni watoto wadogo waje kwangu,msiwazuie,kwa maana watoto kama hawa ufalme wa mungu ni wao.*” Wakati Roho wa Mungu alikuwa akinihudumia kuhusu kubatizwa kwa maji alisema, “Tafuta vifungu ulivyosoma vinavyoonyesha kuwa Mungu ameruhusu watoto wadogo kubatizwa na uniambie”. Huu ni mstari mmoja ambao niliunukuu. “*Wacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazuie, kwa maana watoto kama hawa ufalme wa mungu ni wao*”. Mstari huu unapatikana katika Mariko 10:13-16, Luka 18:15-17 na  Mathayo 19:13-14.

Nilimnukulia Bwana naye akaniambia, “Mwanangu angalia mstari unaofuata nami nikauangalia mstari huo unaosema, “*Yesu akaweka mikono juu yao na kuwabariki*”

Nilizinduka kwa sababu nilifunzwa kuwa neno hili lilidhihirisha ubatizo wa watoto wachanga. Neno hili kamwe halikumaanisha ubatizo huu. Linamaanisha Yesu akawawekea mikono na kuwabariki huku akiwatia wakfu mbele ya Mungu.

Tunaweza kuendelea kufanya yale ambayo hayapatikani katika neno? Twawezaje kuendelea kutumia vifungu kama hivi kuunga mkono jambo ambalo halipatikani katika neno la Mungu. Yesu hakuwabatiza watoto wadogo.

Watoto wadogo hawabatizwi lakini wao hubarikiwa. Inadhihirika kuwa hawakuwaleta kubatizwa bali waliwaleta wabarikiwe.

Makanisa mengi hufikiria kuwa maadam watoto ni sehemu ya mataifa yote, basi wapaswa kubatizwa. Hata hivyo tukisoma kwa makini tunauona ule mstari ukisema "Tuyafunze mataifa tuwafanye wanafunzi kisha tuwabatize". Hapa tunazungumzia wale waliofanyika wanafunzi kwa kulipokea neno la Mungu wala sio mataifa yote. Sisi haturuki tu kwa ndege tukimwagia maji mataifa yote kama inavyofikiriwa hapa.

Ni wale tu ambao wamempokea Yesu na kufanyika wanafunzi wanapaswa kubatizwa kwa maji. Neno 'wote' wa mataifa hakika huwahusu watoto wala sio watoto wachanga. Katika ubatizo wa kweli, watu hupokea na kufunzwa neno la Mungu na kisha hubatizwa kwa utiifu, na imani ambayo Mungu ameikuza katika mioyo yao katika Yesu Kristo. Wanaendelea kutembea na Mungu .

Katika Matendo ya Mitume 2:38, tunaona kuwa mtu anatubu kwanza kisha anabatizwa. Kutubu hutangulia ubatizo. Ni dhahiri kuwa watoto wachanga hawajamwamini Bwana Yesu Kristo na kukiri kwa kinywa vyao kwamba Yesu ndiye Bwana wao.Kukiri kunafanyika wokovu jinsi neno la Mungu linavyosema katika Warumi 10:9-10.

Neno la Mungu hufunza kuwa mtoto anaweza kuamini. Lakini kunayo tofauti kati ya mtoto mchanga na mtoto. Lazima tujue hivi: mtoto anaweza kuamini. (Mathayo 18:6) wakati watoto wanapofunzwa na wazazi wao na kukua wakijua upendo wa Mungu na kipawa cha uzima, wao hutubu na kumuamini Yesu, kukiri kwa vinywa vyao kuwa Yesu Kristo ni Bwana wao, basi huu ndio wakati wao wa kubatizwa bali sio kabla.

## MASWALI NA MAJUKUMU

Hatujapata dhihirisho mwafaka kutoka kwa neno la Mungu linalosema kinyume, Je, kwa watoto wachanga ni jinsi gani? Hapa pia tunaona kama Bwana alivyotuhudumia awali kuwa wazazi wanapaswa kuwaleta watoto wao na kuwatia wakfu mbele za Mungu. Hivyo ndivyo hufanyika watoto hawa wachanga na kimakosa tunasema "wamebatizwa" wakati ambapo "tulibatizwa" tukiwa watoto wachanga, wazazi wetu walikuwa wakituweka wakfu mbele za Mungu. Wazazi walikuwa wakiwatafutia baraka watoto wao na kuahidi kuwa watawafunza watoto wao njia za Mungu huku wakilifuata neno la Mungu pia na kuwa mfano.

Hii inamaanisha kuwa wazazi wanasema kuwa kupitia kwa imani yao watachukua jukumu la kuwafunza watoto njia za Mungu. Neno la Mungu linasema watoto wamo katika baraka za Mungu kwa sababu ya imani ya wazazi wao waanaoamini. (1 Wakorintho 7:14 ) watoto wafikapo umri wa kuamini wao wenyewe, basi wanabatizwa katika mwili wa Bwana yesu Kristo. Pia hakuna umri

uliotengwa. Jambo hili hufanyika wakati mtoto amejifungua mbele za Mungu na kulipokea neno la Mungu

Wao hawabatizwi katika aina fulani ya kanisa kama inavyofikiriwa mara nyingi kimakosa. Wao hubatizwa katika mwili wa Bwana Yesu Kristo wala sio kanisa fulani. (1 Wakorintho 12:12-13, 1 Wakorintho1:13-17, Wagalatia 3:26-29 na Warumi 6:1-4)

Wakati tutakaposimama mbele za Mungu siku moja, kila mmoja atasimama mwenyewe, kivyake, kwa yale tuliyoyafanya kumhusu Bwana Yesu. Imani ya mtu mwingine hitatufunika. Lazima tulipokee neno la Mungu kwa imani na upendo ili tuupate uzima wa milele.

Watu wengi walibatizwa kama watoto wachanga kwa sababu wazazi wao waliogopa kuwa ikiwa lolote linaweza kuwatendekea hawatakuwa na uzima wa Mungu. Marafiki wangu woga ni woga. Vipawa au karama za Mungu husababishwa na upendo. Katika upendo hamna hofu, lakini pendo lililo kamili huitoa nje hofu(Woga). Mungu aliwafanyia njia wale watoto. ( 1Wakorintho 7:14 yasema imani ya mzazi anayeamini hufunika watoto hawa wachanga mpaka wakati ule watakapompokea Bwana yesu. Kutokana na wazazi kutimiza wajibu wao wa kuwatia wakfu watoto hawa na kuwafunza kuujua upendo wa Mungu katika Yesu Kristo. Fikiria jambo hili.

Chunguza moyo wako na maisha yako sasa. Kulifanyika nini kwao?Ulimwagiwa maji kama mtoto mchanga? "Kubatizwa" kama mtoto bila kutubu kwokwote kufanyika katika moyo wako kwa Mungu jinsi neno la Mungu lisemavyo? Je, ulikiri kwa kinywa chako "Yesu ni Bwana" kama ushuhuda dhahiri wa kazi ya Mungu katika maisha yako ulipobatizwa? Je, mzazi au mwakilishi ndiye aliyekufanyia haya?

Neno la Mungu linasema kuwa lazima ukiri kwa kinywa chako, "Yesu Kristo ni Bwana" kwa ubatizo na imani kuwa mwafaka, ulisikia neno la Mungu na kulitenda? "*Imani huja kwa kusikiza neno la Mungu* .(Warumi 10:17)Je imani ilikuwa katika ubatizo wako ulipokuwa mchanga? Ama ulibatizwa kwa sababu mtu mwingine alitaka ubatizwe , kwa hakika ulimjali Mungu? Ikiwa unajua wampenda Mungu, tafuta huduma na upokee kubatizwa kwa maji, ukiri Yesu Kristo ni Bwana katika maisha yako.

Hivi ndivyo kulifanyika katika maisha yangu. Nilitoka katika dhehebu kubwa na kulikuwa na watu waliompenda Mungu. Nawapenda watu hao, nampenda Mungu.Hata hivyo mwanzo kabisa ni kutenda mambo jinsi Mungu anavyosema.Tujitenge na desturi za kidini za mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu. Yesu alisema katika Mathayo 15:9 "*Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu".*

## MANENO YA MWISHO YA KUTIA MOYO

Ninaamini kuwa baada ya kuliangalia neno la Mungu, utafahamu wazi vile Roho wa Mungu alivyodhihiri kwangu. Ubatizo mwafaka lazima uwe na imani iokoayo na kutubu mbele za Mungu.

Nakutia moyo uchunguze moyo wako sasa. Ikiwa hujabatizwa kulingana na kanuni za kimaandiko zilizofanywa na Mungu katika neno lake kuhusiana na ubatizo ufaao basi unatakiwa kubatizwa kwa maji. Haubatizwi tena . Huu ndio ubatizo wako wa kwanza.

Kuna ubatizo mmoja tu wa maji wa kweli. Wakati tulipokuwa watoto, Kwa kumpenda Mungu na pia sisi,wazazi walitukabidhi Bwana na kumuahidi watatulea kulingana na njia zake. Baraka za Mungu ziko juu ya wazazi hao wanaowafundisha watoto wao njia za Bwana.

Mungu ana zawadi ya kipekee kwetu wazazi wakati tunapowahudumia watoto wetu na kuwatunza. Ninaamini kuwa njia moja ya kuwatunza watoto wetu ni kutafuta maandiko sisi wenyewe na kuwafunza watoto wetu hakika anayosema Mungu ili waweze kuwa na ukamilifu wa baraka za Mungu katika maisha yao pia.Mungu atakubariki jinsi alivyoniabariki  utakapolipokea neno lake bila woga na kubatizwa, huku ukimwamini Yesu Kristo kama Bwana wako.

Bwana alinipa mstari ufuatao wa neno wakati nilibatizwa nikimwamini Yesu kama Bwana . Yesu alisema haya kabla ya kubatizwa kwake,”*Kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kutimiza haki yote”*, (Mathayo 3:15)

© 1988, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,
all rights reserved,
www.glorytogod.org